# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.16 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) JUNI 2022

# WALIMU 1,447 WATHIBITISHWA KAZINI, 429 WABADILISHIWA KAZI JANUARI – MACHI, 2022




*Mwenyekiti wa Tume ya utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (katikati) akiongoza Mkutano wa TSC Na. 4/2021/2022 uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma hivi karibuni. Upande wa Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa TSC, Bahati Mgongolwa na upande wa kulia ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama.*

**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

# ASANTE RAIS SAMIA SULUHU HASSAN KWA NYONGEZA YA MISHAHARA KWA WATUMISHI WA UMMA

Hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia mapendekezo ya kuongeza mishahara ikiwemo kima cha chini kwa watumishi wa umma kwa asilimia 23.3, ambapo Shilingi trilioni 1.59 zinatarajiwa kutumika kutokana na ongezeko hilo linaloanzia mwezi Julai 2022.

Uamuzi huo wa Rais Samia ni mwendelezo wa juhudi zake za kuboresha maslahi ya watumishi wa umma toka aingie madarakani mwezi Machi, 2021. Moja ya juhudi kubwa zinazoendelea kukumbukwa na watumishi wa umma ni kuamua kupandisha vyeo wale wote waliokuwa na sifa za kupanda na kumaliza kilio cha watumishi hao kilichokuwa kumedumu kwa muda mrefu.

Kutokana na juhudi hizo, watumishi wa umma wana kila sababu ya kumshukuru Rais Samia kwa maendeleo makubwa anayoleta kwenye Taifa letu ikiwemo kuboresha maslahi ya watumishi wa umma. Tuna wajibu wa kuunga mkono juhudi za Rais wetu kwa kuhakikisha kila mmoja anatimiza wajibu wake katika kutoa huduma kwa wananchi ili jamii na taifa kwa ujumla liweze kufaidi matunda ya kazi inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa upande wa walimu, tuna matumaini kuwa ongezeko hilo la mshahara litakuwa ni chachu ya kuongeza juhudi za kufundisha wanafunzi na kuhakikisha kuwa kiwango cha ufaulu kinazidi kuongezeka kwa kuwa mmoja ya malengo ya Rais Samia ni kuboresha sekta ya elimu na kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama


**Wajumbe**
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania   tumeyautumishiwawalimutanzania

# WALIMU 1,447 WATHIBITISHWA KAZINI, 429 WABADILISHIWA KAZI JANUARI – MACHI, 2022



*Kikao cha Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu ya TSC kikiwa kinaendelea.*

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kupitia wilaya mbalimbali imethibitisha kazini jumla ya walimu 1,447 huku walimu 429 wakibadilishiwa kazi/cheo na mashauri 301 yakihitimishwa katika kipindi cha mwezi Januari hadi Machi, 2022.

Hayo yamebainishwa katika taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu ya TSC katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2021/2022 iliyowasilishwa katika Kamati ya Tume hiyo inayoshughulikia masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu.



*Baadhi ya Maafisa wa TSC ambao ni wajumbe wa Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu ya TSC wakiwa kwenye kikao cha kamati hiyo kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, miongoni mwa kazi za kipaumbele zilizotekelezwa na ofisi za TSC ngazi ya Wilaya katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2021/22 ni kufanya vikao vya kisheria, kuwezesha Kamati za Uchunguzi wa Mashauri ya Nidhamu pamoja na kuwajengea uwelewa Walimu kuhusu masuala ya Utumishi wa Walimu.

Katika kazi ya kufanya vikao vya kisheria, taarifa hiyo ilieleza kuwa katika Robo ya Tatu, Wilaya 128 (92.1%) kati ya 139 ziliwezeshwa kufanya vikao vya kisheria ambapo walimu 1,447 walithibitishwa kazini wakiwemo wa Shule za

# WALIMU 1,447 WATHIBITISHWA KAZINI, 429 WABADILISHIWA KAZI JANUARI – MACHI, 2022

Msingi 902 na Sekondari 545, walimu 429 walibadilishiwa cheo/ kazi wakiwemo 299 wa Shule za Msingi na 130 wa Sekondari, maombi ya kuajiriwa upya walimu 27 yalijadiliwa na kuwasilishwa Tume makao Makuu, mashauri 301 yalihitimishwa kati ya 351 yaliyofunguliwa na mashauri 50 yaliyobaki yapo katika hatua za uchunguzi.

Katika kuwezesha Kamati za Uchunguzi wa Mashauri ya Nidhamu taarifa hiyo ilifafanua kuwa lengo la kazi hiyo ni kuziwezesha Kamati za Uchunguzi kuchunguza tuhuma mbalimbali za walimu walioshtakiwa ili kubaini ukweli wa tuhuma na kuziwezesha



*Katibu wa Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu ya TSC ambaye pia ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kushoto) akiwa katika kikao cha Kamati hiyo, pembeni yake ni Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa TSC, Zachary Dida.*



*Kikao cha Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu ya TSC kikiwa kinaendelea.*

Kamati za Wilaya kutoa uamuzi stahiki huku ikieleza kuwa Wilaya 88 ziliwezeshwa kuchunguza mashauri ya nidhamu 386.

Kwa upande wa kuwajengea uwelewa Walimu kuhusu masuala ya Utumishi wa Walimu, taarifa ilieleza kuwa lengo la kazi hiyo ni kuwawezesha Watumishi wa TSC ngazi ya Wilaya kufanya ziara shuleni na kuwaelimisha walimu kuhusu masuala ya ajira maadili na maendeleo ya kazi ya ualimu.

"Katika Robo ya Tatu, Wilaya 3 za Kilosa, Gairo na Busega ziliwezeshwa kufanya ziara shuleni kuwaelimisha walimu kuhusu masuala ya ajira, maadili na maendeleo ya kazi ya ualimu," ilieleza sehemu ya tarifa hiyo.

# WALIMU 258,291 NA WADAU WENGINE KUNUFAIKA NA TOVUTI MPYA YA TUME BAADA YA WADAU WA AWALI 182,650 KUNUFAIKA NA ILE YA AWALI

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Lazaro Komba, leo katika Mkutano wa Tume amezindua tovuti mpya ya TSC inayotarajiwa kuhudumia Walimu wapatao 258,291 ambao ni Walimu 173,591 wa Shule za Msingi na Walimu 84,700 wa Sekondari tofauti na Wadau mbalimbali 182,650 walionufaika na tovuti ya awali iliyokua na changamoto kadhaa.

Akiongea na washiriki wa hafla ya uzinduzi huo iliyofanyika Jijini



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akitoa hotuba katika hafla ya uzinduzi wa tovuti mpya ya TSC iliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma, Mei 27, 2022.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa maneno ya utangulizi wakati wa hafla ya uzinduzi wa tovuti mpya ya TSC iliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma, Mei 27, 2022.*

Dodona katika Ukumbi wa Chama cha Mapinduzi (Jakaya Kikwete Convention Center) alisema pamoja na kuhudumia walimu, hao tovuti mpya itawahudumia pia wadau wengine wote wa Sekta ya Elimu, Taasisi, Wananchi na Taifa kwa ujumla.

Prof. Komba alisema, "Kwa kipindi cha miaka saba sasa (2017 - 2022) tangu Tume kuwa na tovuti, taarifa na mambo mbalimbali ya TSC ambayo Tume ingependa yawafikie walengwa na jamii kwa ujumla kwa wakati tarajiwa ili kufikia malengo ya utekelezaji zimekua haziwafikii kama ilivyotarajiwa kutokana na changamoto za hapa na pale zilizobainishwa ikiwemo changamoto ya mabadiliko makubwa ya kiteknolojia duniani katika eneo la Habari, Elimu, Mawasiliano na Uhamasishaji.

Aidha, kabla ya kuzindua tovuti hiyo; aliwaelekeza na kuwasisitiza Maafisa TEHAMA na Mawasiliano ya Serikali katika uendeshaji wa tovuti pamoja na zana nyingine zote za mawasiliano na jamii, uhabarishaji, uelimishaji na uhamasishaji ikiwemo mitandao ya jamii, kuzingatia viwango, maelekezo na miongozo yote ya Serikali kwani pamoja na kufuata



*Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Assela Luena akitoa maneno ya shukrani wakati wa hafla ya uzinduzi wa tovuti mpya ya TSC iliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma, Mei 27, 2022.*

# WALIMU 258,291 NA WADAU WENGINE KUNUFAIKA NA TOVUTI MPYA YA TUME BAADA YA WADAU WA AWALI 182,650 KUNUFAIKA NA ILE YA AWALI

maelekezo hayo wamewezeshwa kwa mafunzo kuwa na umiliki wa moja kwa moja wa zana hizo za mawasiliano hali inayosababisha uhuishaji wa taarifa na kufanya maboresho mbalimbali kwa wakati kuwa rahisi.

Hali kadhalika, Prof. Komba alisema kuwa ni matumaini yake kuanzia sasa taarifa zote hai zenye tija kwa Walimu, Wateja, Wadau na Jamii kwa ujumla wake zitapatikana kwa wakati zikiwa hai na zenye tija kwa walengwa ikiwa ni pamoja na kuwezesha wateja kupata huduma muhimu za Tume kupitia tovuti hiyo mpya bila kulazimika kutembelea Ofisi za Tume Makao Makuu au katika Ofisi za Tume ngazi ya Wilaya zote 139.



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa nne kutoka kushoto), Kamishna wa TSC, Assela Luena (wa kwanza kutoka kulia), Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami (wa tatu kutoka kushoto) na Afisa TEHAMA wa TSC, Sophie Michael (wa kwanza kutoka kushoto) wakifurahia uzinduzi wa tovuti mpya ya TSC uliofanyika Mei 27, 2022 jijini Dodoma.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Gerard Chami akitoa taarifa ya tovuti ya TSC wakati wa hafla ya uzinduzi wa tovuti mpya ya TSC iliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma, Mei 27, 2022.*

"Imeelezwa hapa kuwa tovuti mpya iliyoboreshwa itakuwa chanzo sahihi na bora kwa Walimu, Wateja na Wadau mbalimbali wa Sekta ya Elimu kupata taarifa mbalimbali za Tume. Ni wazi taarifa na maudhui yatakayowekwa kwenye tovuti yatatumika kwa usahihi katika kazi mbalimbali ikiwemo kujifunza, kufanya tafiti, kupata huduma na rejea ya nyaraka mbalimbali kuhusu masuala ya Utumishi wa Walimu. Nawasihi wadau wote hususan walimu kuitumia tovuti hii kupata huduma, taarifa, maudhui, takwimu na nyaraka mbalimbali kwa rejea na matumizi sahihi." Alisema Mwenyekiti huyo wa TSC.

Aliwashukuru wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha zoezi la kutengeneza tovuti hiyo iliyogharimu Tzs.6,000,000/= wakiwemo Wadau wa Maendeleo ambao alisema ndiyo msaada na chanzo cha awali cha kuifanikisha Tume kuwa na tovuti, na kipekee aliwashukuru sana Makamishna wa Tume kwa ushirikiano wao, Wajumbe wa Menejimenti ya TSC kwa utekelezaji kwa wakati,

# WALIMU 258,291 NA WADAU WENGINE KUNUFAIKA NA TOVUTI MPYA YA TUME BAADA YA WADAU WA AWALI 182,650 KUNUFAIKA NA ILE YA AWALI








*Baadhi ya washiriki waliohudhuria hafla ya uzinduzi wa tovuti mpya ya TSC iliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma, Mei 27, 2022.*

vilevile Kamati ya TEHAMA ya Tume kwa maoni na ushauri wao, na Idara na Vitengo vyote kwa kuwezesha mchakato wa kumpata mzabuni wa kutekeleza kazi hiyo ikiwa ni pamoja na kuandaa maudhui na taarifa mbalimbali ambazo zitatumika kwenye tovuti hii.

Kwa namna ya pekee Prof. Komba alivipongeza Kitengo cha TEHAMA na Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali vya Tume kwa uratibu wa zoezi zima la matengenezo ya tovuti hiyo kwa pamoja na Watalaam wa TEHAMA kutoka Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP) Ofisi ya Rais TAMISEMI na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kwa ushauri na kazi kubwa ya kutengeneza tovuti na kuwapa mafunzo Maafisa Watalaam wa Tume.

Nae Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, kabla ya

# WALIMU 258,291 NA WADAU WENGINE KUNUFAIKA NA TOVUTI MPYA YA TUME BAADA YA WADAU WA AWALI 182,650 KUNUFAIKA NA ILE YA AWALI



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Makamishna wa TSC pamoja na baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya TEHAMA ya TSC walioshiriki katika mchakato wa kuandaa tovuti mpya ya TSC wakati wa uzinduzi wa tovuti hiyo uliyofanyika Mei 27, 2022 jijini Dodoma. Wengine ni Makamu Mwenyekiti wa TSC, Bi. Bahati Mgongolwa (wa pili kutoka kushoto kwa waliokaa) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia kwa waliokaa).*

kumkaribisha Mwenyekiti wa Tume, Prof. Willy Komba, alizitaja baadhi ya changamoto zilizosababisha maelekezo ya Tume kwa Menejimenti ya Tume kutengenezeza tovuti mpya kuwa ni pamoja na; tovuti ya awali kutengenezwa kwa teknolojia ya zamani, waendeshaji tovuti kutokuwa na uelewa wa kutosha kwenye masuala ya usimamizi wa tovuti hiyo, uhitaji mkubwa wa kuboresha mwonekano na maudhui ya tovuti, uelewa hafifu na usio fasaha wa namna ya kuandaa na kupandisha taarifa, takwimu na nyaraka mbalimbali kwenye tovuti, Maafisa TEHAMA, Habari na Mawasiliano kutokuwa na umiliki wa moja kwa moja (ownership) hali ambayo ilisababisha changamoto katika kuhuisha taarifa na kufanya maboresho mbalimbali kwa wakati, na tovuti kutokidhi mahitaji ya Tume kwa kutokuwa na maeneo ya kutosha kwa ajili ya kuweka taarifa mbalimbali za Taasisi.

Katibu huyo alisema, "Tofauti na tovuti ya awali, tovuti hii mpya ni bora zaidi kwa kuwa; inakidhi mahitaji ya Tume kutokana na uwezo wake wa kubeba taarifa nyingi zaidi kwa wakati mmoja, inaendana na teknolojia ya kisasa, ina uwezo mkubwa wa kuingiza na kupokea maudhui na maboresho ya taarifa kwa wakati, Maafisa wa TSC (TEHAMA na Mawasiliano ya Serikali) kupitia mafunzo yaliyotolewa wana uelewa wa kutosha katika usimamizi



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Makamishna wa TSC pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya TSC wakati wa uzinduzi wa tovuti mpya ya TSC uliyofanyika Mei 27, 2022 jijini Dodoma. Wengine ni Makamu Mwenyekiti wa TSC, Bi. Bahati Mgongolwa (wa pili kutoka kushoto kwa waliokaa) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia kwa waliokaa).*

# WALIMU 258,291 NA WADAU WENGINE KUNUFAIKA NA TOVUTI MPYA YA TUME BAADA YA WADAU WA AWALI 182,650 KUNUFAIKA NA ILE YA AWALI

(administration) na uendeshaji, na tovuti hii inamsaidia mtumiaji (Walimu na wadau wengine wa Tume) kupata viunganishi (links) vya mifumo mingine mbalimbali kwa urahisi."

Akiwasilisha taarifa ya mwenendo wa tovuti ya Tume kabla ya uzinduzi Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa Tume, Gerard Chami, alisema pamoja na faida zilizoainishwa huduma na vitu vitakavyopatikana katika tovuti hiyo mpya ni pamoja na; Ufahamu wa Majukumu ya Tume kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Tume, Sheria ya Tume na Kanuni zake, maelezo na taratibu za upatikanaji wa huduma mbalimbali zitolewazo na Tume, machapisho mbalimbali ikiwemo Miongozo, Mipango Mkakati, Tafiti, Taarifa, Sera, Majarida, Takwimu, Fomu mbalimbali za mtandaoni katika Utumishi wa Umma, na eneo la habari ambamo kutakua na Taarifa mbalimbali kwa Vyombo vya Habari, Hotuba, Vipeperushi, Vibango, Vibonzo, habari picha mnato, habari picha jongefu, Mawasiliano ya Tume pamoja na ramani mtandao ya kufika Ofisi za Tume Makao Makuu, Dodoma na Ofisi za Wilayani zote 139.

Chami alisema vile tovuti mpya iliyoboreshwa itakuwa ni chanzo sahihi na bora cha taarifa mbalimbali kuhusu Tume kwa Walimu, Wananchi, Wadau wa Elimu na Taasisi mbalimbali, Kitengo cha TEHAMA kimejipanga vema kusimamia kikamilifu tovuti hiyo ili iweze kufanya kazi na kupatikana kwa muda wote huku Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali nacho kikiahidi kuhuisha taarifa kwa wakati na kwa kadri zinavyohitajika kwa walaji ili wadau wote waweze kupata taarifa kwa wakati na waweze kutumia huduma zilizopo kwenye tovuti hiyo.



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Makamishna wa TSC pamoja na baadhi ya watumishi wa TSC wakati wa uzinduzi wa tovuti mpya ya TSC uliyofanyika Mei 27, 2022 jijini Dodoma. Wengine ni Makamu Mwenyekiti wa TSC, Bi. Bahati Mgongolwa (wa pili kutoka kushoto kwa waliokaa) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia kwa waliokaa).*

Kamishna Assela Luena akitoa neno la shukrani kwa niaba ya Makamu Mwenyekiti wa Tume, Kamishna Bahati Mgongolwa, alisema kukamilika kwa tovuti mpya ni jambo la kheri, lenye tija na manufaa makubwa kwa Tume na Taifa kwa ujumla wake kwani inaenda kuhudumia sehemu kubwa zaidi ya wateja wa TSC hususan Walimu, Wadau wa Elimu, Watafiti, Taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi pamoja na Wananchi kwa ujumla na kupunguza uhaba wa awali wa upatikanaji wa taarifa mbalimbali muhimu kwa wateja wa Tume.

Hafla hiyo ya uzinduzi wa tovuti mpya ya Tume ulihudhuriwa na Waheshimiwa Makamishna wa Tume, Katibu wa Tume, Wajumbe wa Menejimenti ya Tume, Wajumbe wa Kamati ya TEHAMA ya Tume, Mtaalamu mwakilishi kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Sekretarieti ya Mkutano wa Tume, Wanahabari na Watumishi wa Tume.

# TSC YAAMUA RUFAA 49 ZA WALIMU, YATEUA WAJUMBE 37 KAMATI ZA WILAYA



*Mwenyekiti wa Tume ya utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (kulia) akiongoza Mkutano wa TSC Na. 4/2021/2022 uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma hivi karibuni. Pembeni yake ni Makamu Mwenyekiti wa TSC, Bahati Mgongolwa.*

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Januari hadi Machi, 2022 Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeamua rufaa 49 za walimu waliopinga uamamuzi uliotolewa na TSC ngazi ya Wilaya na hivyo kufanya jumla ya rufaa 193 katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Hayo yameelezwa katika taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2021/2022 inayoanzia mwezi Januari hadi mwezi Machi, 2022 iliyowasilishwa katika Kamati ya Tume ya Maadili na Nidhamu ya Walimu kwa ajili ya kuwasilishwa Mkutano wa Tume Na. 4/2021/2022 uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma hivi karibuni.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa katika rufaa 193 zilizoamuliwa, rufaa 53 zilitolewa uamuzi kwenye Mkutano wa Tume Na. 1/2021/22, rufaa 45 zilitolewa uamuzi kwenye Mkutano Na.2/2021/22, rufaa 49 zilitolewa uamuzi kwenye Mkutano wa Tume Na.3/2021/22 na Rufaa 46 ziliamuliwa katika Mkutano Na.4/2021/22.

Pamoja na kushughulikia rufaa hizo, TSC imefanikiwa kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za TSC ngazi ya Wilaya wa Kanda ya Kaskazini na Kusini katika mafunzo yaliyofanyika tarehe 5 – 6 Aprili, 2022 Jijini Dodoma ambapo yalihusisha jumla ya Wajumbe 106 kutoka Mikoa ya Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Mtwara, Lindi na Ruvuma.

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2022 TSC pia imefanikiwa kufanya ufuatiliaji katika Wilaya 10 za Songwe, Mbozi, Ileje, Momba, Kahama, Shinyanga, Kishapu, Singida, Manyoni na Ikungi kwa lengo kuona kama Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu inazingatiwa katika kusimamia na kushughulikia masuala yanayohusu Utumishi wa Walimu.

Vilevile, ufuatiliaji huo ulikusudia kufanya tathmini ya mafunzo yaliyotolewa kwa Wajumbe wa Kamati ngazi ya Wilaya kuona kama yameleta tija katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya Tume ambapo imebainika kuwa mafunzo yaliyotolewa kwa Wajumbe wa Kamati kwa kiasi kikubwa yameboresha utendaji kazi wa ofisi hizo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, TSC imeendelea kufanya kazi ya Uandishi wa uamuzi wa rufaa na maagizo ya mbalimbali ya Tume ambapo lengo la kazi hiyo ni uandishi wa uamuzi wa rufaa, maagizo ya Tume na Mihtasari ya Mikutano ya Tume ili kuhakikisha kuwa Warufani wanapata uamuzi



*Mkutano wa TSC Na. 4/2021/2022 ukiwa unaendelea.*

# TSC YAAMUA RUFAA 49 ZA WALIMU, YATEUA WAJUMBE 37 KAMATI ZA WILAYA

wa rufaa ndani ya siku 21 tangu ulipotolewa na Tume kwa mujibu wa Sheria.

Kazi nyingine iliyofanyika katika kipindi gicho ni kuandaa taarifa, vielelezo na mwenendo wa rufaa vya Warufani waliokata rufaa kwa Rais dhidi ya uamuzi wa Tume ambapo rufaa 12 za warufani waliokata rufaa kwa Rais dhidi ya uamuzi wa Tume zilipokelewa na kati ya hizo taarifa za mwenendo na vielelezo vya rufaa nane (8) ziliandaliwa na kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi na rufaa nne (4) zipo katika hatua ya uchambuzi.

Sambamba na kupokea taaarifa hiyo, Mkutano huo pia umefanya uteuzi wa kujaza nafasi 37 za Wajumbe wa Kamati za TSC kutoka Wilaya 28 ili kujaza nafasi za wajumbe waliokosa sifa kuendelea na nafasi hizo kutokana a sababu mbalimbali ikiwemo uhamisho wa nje ya wilaya husika, kupata uteuzi na kustaafu.

Nafasi zilizojazwa ni; Wenyeviti 6 kutoka Wilaya za Kasulu, Momba, Songwe, Karatu, Mbinga na Nyasa; Wajumbe 16 wa Shule za Msingi na Sekondari kutoka Wilaya za Kasulu, Mvomero, Kiteto, Sumbawanga, Songwe, Dodoma, Nachingwea, Karatu, Handeni, Handeni, Mwanga, Singida, Iramba, Monduli na Nyang'wale.

Wajumbe wengine walioteuliwa ni Maafisa Elimu 11, kutoka Wilaya za Kasuli, Ileje, Ikungi,Uvinza,Bunda,Nyamagana, Buhigwe, Biharamulo, Kilindi, Nyasa na Singida pamoja na Makatibu Tawala 3 kutoka Wilaya za Songwe, Liwale na Kilwa.



*Kikao cha Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kikiwa kinaongozwa na Kamishina wa TSC, Mwamgeni Jongo.*



*Katibu wa Kamati ya Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akitoa ufafanuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Tume katika Eneo la Maadili na Nidhamu ya Walimu.*



*Kikao cha Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kikiwa kinaongozwa na Kamishina wa TSc, Mwamgeni Jongo.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia) akiongoza kikao cha awali (entrance Meeting) kati ya Menejimenti ya TSC na Wakaguzi wa Nje kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ikiwa ni mwanzo wa kuanza shughuli za ukaguzi. Kikao hicho kimefanyika hivi karibuni katika ukumbi wa Mikutano wa TSC jijini Dodoma.*



*Afisa kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) (katikati) akitoa maelezo wakati wa kikao cha awali (entrance Meeting) kati ya Menejimenti ya TSC na Wakaguzi kutoka ofisi ya CAG kilichofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa TSC jijini Dodoma hivi karibuni.*



*Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi wa TSC, Lameck Mbeya akitoa maelezo wakati wa kikao cha awali (entrance Meeting) kati ya Menejimenti ya TSC na Wakaguzi kutoka ofisi ya CAG kilichofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa TSC jijini Dodoma hivi karibuni.*



*Kikao cha awali (entrance Meeting) kati ya Menejimenti ya TSC na Wakaguzi wa Nje kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kikiwa kinaendelea. Kikao hicho kimefanyika hivi karibuni katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC jijini Dodoma.*





*Kikao cha awali (entrance Meeting) kati ya Menejimenti ya TSC na Wakaguzi wa Nje kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kikiwa kinaendelea. Kikao hicho kimefanyika hivi karibuni katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC jijini Dodoma.*

# VIONGOZI TSC WATEMBELEA ENEO LA KIWANJA CHA TUME HIYO NJEDENGWA, DODOMA



*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Zachary Dida akiwaonesha viongozi wa TSC kiwanja cha TSC kilichopo eneo la Njedengwa jijini Dodoma (hakionekani pichani) ambapo maandalizi ya kuanza kwa ujenzi wa jengo la ofisi za TSC Makao Makuu yameanza.*

**Na Mwandishi wetu – Dodoma**

Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiongozwa na Mwenyekiti na Katibu wa Tume hiyo wametembelea kiwanja cha TSC kilichopo eneo la Njedengwa jijini Dodoma ambapo maandalizi ya kuanza kwa ujenzi wa ofisi za Tume Makao Makuu yanendelea kufanyika.

Viongozi hao walifanya ziara hiyo Mei 25, 2022 kwa lengo la kufahamu eneo hilo na kujionea hatua iliyofikiwa katika hatua za awali za maandalizi ya kuanza kwa ujenzi huo ambapo walimkuta mkandarasi akiendelea na kazi ya kusafisha eneo huku baadhi ya vifaa vya kazi vikiwa vimefikishwa kwenye eneo hilo.

Akiwa katika eneo hilo, Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba alimweleza Mkandarasi kutoka SUMA JKT ambao ndio wanaojenga jengo hilo kuwa TSC inatarajia kuwa ujenzi huo utakwenda kwa kasi ili ukamilike katika kipindi kilichopangwa.

"Mimi na Makamishna wenzangu tumeteuliwa kushika nafasi hizi kwa kipindi cha miaka mitatu, na tunatamani tuone ofisi za Tume zinajengwa kabla muda wetu haujamalizika. Hivyo, nikuombe Mkandarasi hakikisheni ujenzi huu unakwenda kwa kasi kwa kuwa malipo ya awali tayari tumeshawalipa, hakuna sababu inayofanya ujenzi huu usiende kwa wakati," alisema.

Mwenyekiti huyo alieleza kuwa ameridhishwa kuona kuwa shughuli za kusafisha kiwanja zimeanza na baadhi ya vifaa tayari vimewasili kwenye eneo hilo, hivyo anatarajia kuwa kazi ya rasmi ya ujenzi itaanza katika kipindi cha muda mfupi.

"Ninashukuru kuona kuwa angalau sasa kuna dalili kwamba muda si mrefu ujenzi rami wa



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akisisitiza jambo wakati viongozi wa TSC walipotembelea kiwanja cha TSC kilichopo Njedengwa jijini Dododma kwa ajili ya kujionea jinsi maandalizi ya kuanza kwa ujenzi wa ofisi za TSC Makao Makuu unavyoendelea, ziara ya viongozi hao ilifanyika hivi karibuni.*

# VIONGOZI TSC WATEMBELEA ENEO LA KIWANJA CHA TUME HIYO NJEDENGWA, DODOMA



*Mhandisi kutoka SUMA JKT anayesimamia ujenzi wa jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu katika eneo la Njedenngwa jijini Dodoma akitoa ufafanuzi kuhusu kuanza kwa shughuli za ujenzi huo. Alitoa ufafanuzi huo wakati wa ziara ya viongozi wa TSC iliyofanyika katika eneo hilo hivi karibuni.*

jengo utaanza. Ninaona tayari mmesafisha uwanja na mmeanza kuleta vifaa, ninachowaomba pamoja na kwamba huenda mna kazi nyingi za ujenzi hakikisheni ujenzi huu mnaupatia kipaumbele ili walimu waweze kuhudumia katika mazingira bora," alisema Prof. Komba.

Kwa upande wake Katibu wa TSC, Paulina Nkwama alisema kuwa TSC itaendelea kufuatilia kwa karibu ujenzi huo na kuhakikisha kwamba kazi hiyo inafanyika kwa kasi na kwa ubora ili serikali iweze kufikia malengo yake katika kutoa huduma kwa walimu.

Aliongeza kuwa, katika bajeti ya 2021/2022 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni mia tano (500,000,000) kwa ajili ya kuanza kwa ujenzi huo ambapo shilingi 383,000,000.00 zimeshalipwa kwa SUMA JKT kwa ajili ya kuanza shughuli za ujenzi huo.

"Kuanzia sasa ziara za kuja hapa hazitakoma, tutakuja mara kwa mara ili kuona namna ujenzi huu unavyokwenda. Tunamshukuru sana Rais wetu, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha za kuanza kwa ujenzi huu na ni imani yetu kuwa ataendelea kutupatia fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huu," alisema Katibu huyo.

Naye Mkandarasi kutoka SUMA JKT amewahakikishia viongozi hao wa TSC kuwa kazi hiyo itafanyika kwa kasi ili kuendana na muda uliowekwa huku akisisitiza kuwa watawashirikisha TSC kwa kila hatua ya ujenzi ili kuhakikisha jengo linalojengwa linakidhi matarajio.



*Viongozi wa TSC wakipitia ramani ya kiwanja cha Tume hiyo wakati walipofanya ziara katika eneo la Njedengwa hivi karibuni.*



*Sehemu ya kiwanja cha TSC ambayo inaendelea kusafishwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ofisi za TSC Makao Makuu.*



*Baadhi ya vifaa vikiwa vimefikishwa kwenye kiwanja cha TSC kwa ajili ya kuanza shughuli za ujenzi wa jengo la ofisi za TSC katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma.*



*Kamishna wa TSC, Susana Nussu akimuonesha jambo Kamishna Assela Luena wakati wa ziara ya viongozi hao iliyofanyika hivi karibuni katika kiwanja cha TSC kilichopo Njedengwa jijini Dodoma.*



*Picha ya pamoja ya viongozi wa TSC wakiongozwa na Mwenyekiti wa Tume, Prof. Willy Komba (wa nne kutoka kushoto mstari wa mbele) wakati wa ziara yao katika kiwaja cha TSC kilichoko eneo la Njedengwa jijini Dodoma. Pichani, wa kwanza kutoka kulia ni Mhandisi anayesimamia mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi za TSC kutoka SUMA JKT.*

# WALIMU 612 WASTAAFU KAZI KATIKA KIPINDI CHA JANUARI – MACHI, 2022



*Mwenyekiti wa Tume ya utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (katikati) akiongoza Mkutano wa TSC Na. 4/2021/2022 uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma hivi karibuni. Upande wa Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa TSC, Bahati Mgongolwa na upande wa kulia ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama.*



*Makamishna wa TSC, Jane Mtindya (kushoto) na Huruma Mageni wakiwa kwenye Mkutano wa TSC Na. 4/2021/2022 uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma hivi karibuni.*

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeeleza kuwa jumla ya walimu 612 wanaofundisha shule za Msingi na Sekondari za Serikali Tanzania Bara wamestaafu kazi katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2021/2022 ambacho kinaanzia mwezi Januari hadi Machi 2022.

Hayo yamebainika katika taarifa ya TSC ya utekelezaji wa Majukumu ya Tume hiyo katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2021/2022 iliyotolewa katika Mkutano wa Tume hiyo Na. 4/2021/22 uliofanyika jijini Dododma hivi karibuni ambapo ilibainisha kazi mbalimbali zilizotekelezwa na TSC katika kipindi hicho.



*Makamishna wa TSC, Optat Mrina (kulia) na Mwamgeni Jongo wakiwa kwenye Mkutano wa TSC Na. 4/2021/2022 uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma hivi karibuni.*

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa katika walimu 612 waliostaafu kazi, walimu 557 ni wa shule za msingi na walimu 55 ni wa shule za Sekondari huku ikielezwa kuwa wengi wao walistaafu kwa lazima baada ya kufikia umri wa miaka 60 ambao ndio ukomo wa utumishi huo kwa mujibu wa sheria na huku wengine wakistaafu kwa hiari baada ya kufikia umri wa miaka 55.

"Katika kipindi hicho walimu wa shule za msingi 438 walistaafu kwa lazima,119 walistaafu kwa hiari. Kwa upande wa shule za Sekondari walimu 42 waliostaafu kwa lazima, 13 kwa hiari" ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Pamoja na kustaafu kazi, taarifa hiyo ilieleza kuwa jumla

# WALIMU 612 WASTAAFU KAZI KATIKA KIPINDI CHA JANUARI – MACHI, 2022



*Washiriki wa Mkutano wa TSC Na. 4/2021/2022, Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mectildis Kapinga (kushoto) na Mkurugenzi Msaidizi wa Maadili na Nidhamu wa TSC, Robert Lwikolela wakiwa kwenye Mkutano huo uliofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

walimu 127 walihitimisha kazi kwa kufariki dunia ambapo katika idadi hiyo walimu 91 ni wa shule za msingi na walimu 36 ni wa shule za sekondari.

TSC pia ina jukumu la kuchambua madai yanayohusiana na Mikataba, Mirathi na Pensheni ya kabla ya tarehe 1.7.2004 na kuyawasilisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa uhakiki na Hazina kwa malipo.

Katika kipindi cha Januari – Machi, 2022 jumla ya majalada 45 ya Mikataba, Mirathi na Pensheni yalifanyiwa kazi ambapo kati ya hayo majalada 24 yaliandaliwa na kupelekwa kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Majalada 21 yaliandaliwa na kupelekwa Hazina kwa ajili ya malipo. Aidha, wanufaika 23 walilipwa mafao ambapo kati yao 12 ni Mikataba, 6 ni Pensheni na 5 ni Mirathi.

Taarifa hiyo iliendelea kufafanua kuwa kazi nyingine zilizotetekelezwa na TSC katika eneo la ajira na maendeleo ya walimu ni usajili wa walimu pamoja na kuajiriwa kwa Walimu 114 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka huo wa fedha ambao kati ya hao, Walimu 28 niwa Shule za Msingi na 86 Shule za Sekondari huku jumla ya Walimu 169 wakisajiliwa ambapo kati yao Walimu 116 ni wa Shule za Msingi na Walimu 53 ni wa Shule za Sekondari.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi 2022, Walimu wanaofundisha kwa Mkataba ni 64 ambapo katika idadi hiyo walimu 51 ni wa Shule za Msingi na walimu 13 ni wa shule za Sekondari.





*Mkutano wa TSC Na. 4/2021/2022 ukiwa unaendelea.*

# TSC YATEKELEZA AGIZO LA WAZIRI NAPE, UHUISHAJI WA TOVUTI ZA SERIKALI



*Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye akizungumza na Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serikalini wakati akifungua kikao kazi cha 17 cha Maafisa hao kinachofanyika Jijini Tanga.*

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imetekeleza agizo la Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape Nnauye la kuwataka Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano wa Serikali kuhuisha taarifa za Serikali kwenye tovuti za Serikali na mitandao ya kijamii ili wananchi waweze kupata taarifa na kujua kinachoendelea kuhusu Serikali yao.

Agizo hilo hivi karibuni akiwa jijini Tanga wakati akifungua Kikao cha 17 cha Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano wa Serikali ambapo alieleza kuwa Maafisa Habari wa Serikali ni daraja linalorahisisha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi, hivyo ni muhimu kutimiza wajibu wao kwa kuwa na taarifa sahihi za Serikali na kwa wakati katika tovuti za Wizara au Taasisi zao.

"Natoa siku 14 kuanzia Mei 14 mwezi huu kila tovuti ya Serikali na mitandao ya kijamii iwe na taarifa za Serikali zinazoendana na wakati kuhusu utekelezaji wa Sera au miradi mbalimbali ya Serikali", alisema Mheshimiwa Nape.

Agizo hilo lilikuja wakati TSC ikiwa imekalisha utengenezaji wa tovuti mpya ya ofisi hiyo ambayo ni ya kisasa zaidi inayoendanda na Miongozo ya Serikali pamoja na teknolojia ya sasa huku ikiwa na uwezo wa kuchukua taarifa nyingi zaidi tofauti na tovuti iliyokuwepo awali.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa tovuti hiyo uliofanyika hivi karibuni jijini Dodoma, Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba aliwataka Maafisa TEHAMA na Mawasiliano ya Serikali ambao ndio wanaouhusika na usimamizi na uendeshaji wa



*Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serikalini wakifuatilia hotuba ya Mgeni rasmi Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye (hayupo pichani) wakati wa Ufunguzi wa kikao kazi cha 17 cha Maafisa hao kinachofanyika Jijini Tanga.*

# TSC YATEKELEZA AGIZO LA WAZIRI NAPE, UHUISHAJI WA TOVUTI ZA SERIKALI



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akitoa hotuba katika hafla ya uzinduzi wa tovuti mpya ya TSC iliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma, Mei 27, 2022.*

tovuti hiyo kuhakikisha tovuti hiyo inapatikana wakati wote na inakuwa na taarifa hai ili kuwasaidia wadau mbalimbali kupata taarifa za TSC kwa urahisi.

"Imeelezwa hapa kuwa tovuti mpya iliyoboreshwa itakuwa chanzo sahihi na bora kwa Walimu, Wateja na Wadau mbalimbali wa Sekta ya Elimu kupata taarifa mbalimbali za Tume. Ni wazi taarifa na maudhui yatakayowekwa kwenye tovuti yatatumika kwa usahihi katika kazi mbalimbali ikiwemo kujifunza, kufanya tafiti, kupata huduma na rejea ya nyaraka mbalimbali kuhusu masuala ya Utumishi wa Walimu. Nawasihi wadau wote hususan walimu kuitumia tovuti hii kupata huduma, taarifa, maudhui, takwimu na nyaraka mbalimbali kwa rejea na matumizi sahihi." Alisema Mwenyekiti huyo wa TSC.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa maneno ya utangulizi wakati wa hafla ya uzinduzi wa tovuti mpya ya TSC iliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma, Mei 27, 2022.*

Nae Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, alisema kuwa lengo la TSC ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa kwa wakati hivyo baada ya kuona tovuti ya awali haikidhi viwango ofisi yake iliamua kutengeneza tovuti mpya ili kuendana na kasi ya utendaji wa kazi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kutoa kutoa taarifa kwa wananchi.

Maafisa Habari kutoka TSC nao walikuwa miongoni mwa maafisa walioshiriki Kikao kazi hicho cha 17 cha Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano wa Serikali kilichofanyika kwa siku tano kuanzia Mei 09-13, 2022 jijini Tanga.

# TSC YAPANDISHA VYEO JUMLA YA WALIMU 1,566 WILAYANI IRINGA, MUFINDI NA KILOLO



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Iringa wakati wa ziara yake aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*

**Na. Mwandishi Wetu – Iringa**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imepandisha jumla ya Walimu 1,566 katika wilaya tatu mkoani Iringa ikiwamo Mufindi, Kilolo na Iringa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 ikiwa ni utekelezaji wa maagizo na maelekezo ya Serikali katika kuboresha na kuimarisha maslahi ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchini.

Hilo limebainika katika taarifa ya ziara ya kawaida ya Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, mara baada ya ziara hiyo iliyofanyika mkoani Iringa hivi karibuni katika wilaya za Mufindi, Kilolo na Iringa, ikiwa ni mwendelezo wa ziara za usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Tume wilayani pamoja na kutoa elimu



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (mwenye miwani) akizungumza na watumishi wa TSC Wilaya ya Mufindi wakati wa ziara yake aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*

# TSC YAPANDISHA VYEO JUMLA YA WALIMU 1,588 WILAYANI IRINGA, MUFINDI NA KILOLO



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Kilolo wakati wa ziara yake aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*

zaidi ya uelewa wa majukumu ya TSC.

"Lengo kuu la ziara hii ya ufuatiliaji lilikua ni kujiridhisha na uzingatiwaji wa maelekezo ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (KM, OR - MUUUB) katika zoezi la kuwapandisha na kuwabadilisha vyeo watumishi walimu. Aidha, malengo mahususi yalikua ni pamoja na kubaini iwapo maelekezo yaliyotolewa na KM, OR - MUUUB yaliwafikia Makatibu Wasaidizi na kama waliyatekelezwa kwa ufasaha; kubaini iwapo vikao vya kamati vilifanyika katika kuwapandisha na kuwabadilisha vyeo watumishi walimu; kupitia takwimu zilizowasilishwa Makao Makuu - TSC ikilinganishwa na hali halisi ya takwimu zilizopo wilayani zinazohusu zoezi la kuwapandisha na kuwabadilisha vyeo watumishi walimu; kufahamiana na watumishi na kuona hali halisi na mazingira yao wanayofanyia kazi." Ilisema taarifa hiyo ya Katibu wa Tume

Taarifa hiyo ilionyesha takwimu za Walimu waliopandishwa madaraja kwa kila wilaya ambapo kwa Wilaya ya Iringa walimu waliopandishwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ni 277, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ni 507, kwa upande wa Wilaya ya Mufindi, Halmashauri ya Mji Mafinga ilipandisha walimu 78 na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilipandisha Walimu 379.

Kwa upande wa Wilaya ya Kilolo taarifa hiyo ilieleza kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo Walimu 325 walipandishwa huku walimu 36 wakibadilishiwa muundo wa utumishi na kazi hiyo bado inaendelea.

Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu katika Wilaya ya Iringa inahudumia Halmashauri mbili za Iringa Manispaa na Iringa; huku Tume ya Utumishi wa Walimu katika Wilaya ya Mufindi ikihudumia Halmashauri mbili ya Mafinga Mji na Mufindi; na Ofisi za Tume Wilaya ya Kilolo inahudumia Halmashari moja ammbayo ni ile ya Wilaya ya Kilolo.

# TSC YAWAJENGEA UWEZO WAKUFUNZI NA WANACHUO WA CHUO KIKUU CHA KIISLAM CHA MOROGORO

**Na Mwandishi wetu – Morogoro.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imewajengea uwezo wakufunzi na Wanachuo wa Chuo Kikuu cha Kiislam cha Morogoro juu ya Sheria, Kanuni na taratibu mbalimbali zinazohusu Utumishi wa walimu.

Hayo yamefanyika Mei 27, 2022 katika mkutano kati ya TSC na wadau hao wa elimu kufuatia TSC kupata mwaliko wa kutembelea na kuzungumza na wadau hao chuoni hapo.

Wakiwa chuoni hapo, Maafisa wa TSC walipata fursa ya kuzingumzia masuala mbalimbali ikiwemo majukumu yanayotekelezwa na TSC, Ajira na Maendeleo ya Walimu, Maadili na Maendeleo ya Walimu, haki na wajibu wa mwalimu pamoja na



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Morogoro, Lusubilo Mwaisunga akiwasilisha mada kwa wakufunzi na wanachuo wa Chuo Kikuu cha Kiislam cha Morogoro (hawapo pichani) wakati wa ziara iliyofanyika chuoni hapo hivi karibuni.*



*Afisa wa TSC kutoka Makao Makuu, Neema Lemunge akiwasilisha mada kwa wakufunzi na wanachuo wa Chuo Kikuu cha Kiislam cha Morogoro (hawapo pichani) wakati wa ziara iliyofanyika chuoni hapo hivi karibuni.*



*Afisa wa TSC kutoka Makao Makuu, Laurence Chankan akiwasilisha mada kwa wakufunzi na wanachuo wa Chuo Kikuu cha Kiislam cha Morogoro (hawapo pichani) wakati wa ziara iliyofanyika chuoni hapo hivi karibuni.*

# TSC YAWAJENGEA UWEZO WAKUFUNZI NA WANACHUO WA CHUO KIKUU CHA KIISLAM CHA MOROGORO



*Mmoja wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kiislam cha Morogoro akichangia mada wakati wa mkutano wa wanachuo hao na maafisa kutoka TSC (hawapo pichani) uliofanyika hivi karibuni mjini Morogoro.*



*Mmoja wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kiislam cha Morogoro akichangia mada wakati wa mkutano wa wanachuo hao na maafisa kutoka TSC (hawapo pichani) uliofanyika hivi karibuni mjini Morogoro.*

kuwashauri wanafunzi wa chuo hicho hususan wa Kitivo cha Elimu kuhakikisha wanazingatia Miiko na Maadili ya taaluma ya ualimu ili wawe walimu bora wenye tija kwa Taifa lao.

Katika ziara hiyo, maswali mbalimbali yaliulizwa na kutolewa ufafanuzi na maafisa wa TSC, Bibi Neema Lemunge, Bw. Laurence Chankan kutoka TSC Makao Makuu pamoja na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Morogoro, Bibi Lusubilo Mwaisunga.

Mingoni mwa masuala yaliyoulizwa na kutolewa majibu ni; baadhi ya Waajiri kutokugharamia mafunzo ya wanachuo waliowekwa kwenye Mpango wa Mafunzo; Changamoto ya Mwalimu anayebadilishiwa cheo baada ya kujiendeleza; wajibu wa Tume katika kuhakisha mafao ya wastaafu yanalipwa kwa wakati pindi wanapostaafu na faida ya mwalimu kujiendeleza kielimu katika hatua ya Uzamili na Uzamivu kwa kuwa hazitambuliki kwenye Muundo wa Walimu.



*Baadhi ya wanachuo wa Chuo Kikuu cha Kiislam cha Morogoro waliohudhuria mkutano wao na maafisa kutoka TSC uliofanyika hivi karibuni mjini Morogoro.*



*Baadhi ya wanachuo wa Chuo Kikuu cha Kiislam cha Morogoro waliohudhuria mkutano wao na maafisa kutoka TSC uliofanyika hivi karibuni mjini Morogoro.*

# TSC YASHIRIKI MAFUNZO YA MFUMO WA USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU KATIKA OFISI ZA UMMA

**Na Mwandishi wetu – Dodoma.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeshiriki mafunzo ya mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu katika ofisi za umma yaliyofayika kwa siku tatu, Mei 23-25 katika Ukumbi wa ofisi ya Jeshi la Zimamoto jijini Dodoma.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na yalilenga kuwajengea uwezo watumishi ambao sio wa kada ya Utumishi na Utawala kuuelewa mfumo huo na kuutumia hasa katika kipengele cha usimamizi wa malimbikizo ya madai ya mshahara na stahili mbalimbali za watumishi wa umma.

Washiriki wa Mafunzo hayo walikuwa ni Wakaguzi wa Ndani na Wahasibu huku TSC ikiwakilishwa na; Bw. Revocatus Misonge, Mhasibu Mkuu; Bibi Grace Mrema, Mkaguzi Mkuu wa Ndani; Bw. Tomas Tambilija, Mkaguzi wa Ndani; na Bw. Mashaka Athuman, Mhasibu.

Taarifa ya washiriki hao kutoka TSC ilieleza kuwa miongoni mwa mafanikio waliyoyapata katika mafunzo hayo ni kufahamu mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali watu (HCIMIS) katika Taasisi za serikali na kupata uelewa wa namna ya kushughulikia malimbikizo ya mishahara na stahili kupitia mfumo (Arreas management).

Mafanikio mengine ya mafunzo hayo ni kujifunza namna ya uanzishwaji wa Taasisi (Estblishment), namna ya kuajiri (Employment) watumishi, namna ya kumsimamia mtumishi tangu anapoajiriwa mpaka anapohitimisha utumishi wake, namna ya kupata taarifa mbalimbali za watumishi kupitia mfumo pamoja na sababu zinazoweza kusababisha kutokea kwa malimbikizo ya mishahara au stahili za watumishi.



**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania